


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA BUKOMBE



13/10/2021

**UFAFANUZI WA HABARI ILIYOCHAPISHWA KATIKA TOVUTI YA
MWANANCHI COMMUNICATION LTD www.mwananchi.co.tz KUHUSU
WANAWAKE 62 WAMEBAINIKA KUWA WANAMAAMBUKIZI YA VVU.**

Katika tovuti ya Mwananchi Communication LTD www.mwananchi.co.tz siku ya Jumapili tarehe 10 Oktoba 2021 ilichapishwa habari kwamba Mkuu wa Wilaya ya Bukombe Mhe. Said Nkumba amesema kuwa wanawake 62 wamebainika kuwa na maambukizi ya Virusi vya Ukimwi (VVU) wakati akitoa taarifa ya upimaji wa VVU ya usiku wa mkeshwa wa Mbio za Mwenge Maalumu wa Uhuru Mjini Ushirombo.

Taarifa hiyo siyo ya kweli. Ifahamike kuwa wateja waliojitokeza kupima Virusi vya Ukimwi wakati wa mkeshwa wa Mwenge wa Uhuru Wilaya ya Bukombe ni 437, wanaume 375 na wanawake 62. Jumla ya waliogundulika na maambukizi ni watu 2, wanaume 0 na wanawake 2.

Katika mwaka wa fedha 2020/2021 Wilaya ya Bukombe ilifanikisha zoezi la upimaji wa VVU kwa wateja 19,572 kati yao wanaume ni 7,484 na wanawake 12,088. Wateja 1,647 walibainika kuwa na maambukizi ya VVU kati yao wanawake 964 sawa na asilimia 4.92 na wanaume 683 sawa na asilimia 3.52. Wateja hawa wameunganishwa kwenye huduma za tiba na matunzo. Hali ya maambukizi kiwilaya ni asilimia 4.9.

Wilaya ya Bukombe inatoa dawa za kufubaza Virusi kwa watu 9398 wanaoishi na maambukizi ya VVU kwa kushirikiana na wadau wa sekta ya Afya ambao ni MDH, ICAP, NELICO, NACOPHA na SHIDEPHA katika kutekeleza Afua zinazolenga kupambana na maambukizi ya VVU na Kifua kikuu kwa wananchi.

Imetolewa na:

Atupakisye M. Mwakalembusya

Atupakisye M. Mwakalembusya

Afisa Habari

Halmashauri ya Wilaya ya Bukombe.

**Kny. MKURUGENZI MTENDAJI <W
BUKOMBE.**